# Haki Zako za Elimu

## Haki ni Nini?

Nchini Marekani, shule na familia hufanya kazi pamoja ili kuwasaidia watoto kujifunza na kukua. Kuna sheria za kuhakikisha kwamba kila mtoto anapata elimu bora. Haki na ulinzi uleule wa shule za umma hutumika kwa wanafunzi na familia zote. Wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha mpya wana ulinzi unaohusiana na kupokea misaada ya lugha na kuweza kushiriki katika shughuli zote za shule. Haki hizi huhakikisha kwamba wanafunzi wana utegemezo wanaohitaji ili kufikia programu na fursa zilezile zinazotolewa kwa wanafunzi wote. Wanafunzi hawapaswi kuachwa nje ya shughuli za shule, mitaala, na programu kwa sababu wanachukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza.

> Wanafunzi wa Kiingereza ni wanafunzi waliopata alama chini ya kiwango cha ustadi katika Kiwamba cha Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio au Tathmini ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio.

Familia zinapaswa kuelewa haki za wanafunzi wao. Kisha, watambue wanachotarajia kutoka kwa shule yao. Wanaweza kuhakikisha kwamba wanapata elimu bora iwezekanavyo. Hili husaidia kuwatayarisha wanafunzi kwa ajili ya wakati ujao mwangavu.

## Haki za Kuwasiliana na Shule

Watoto hufanikiwa zaidi familia na shule zinapofanya kazi pamoja. Ili kufanya hivi, ni lazima familia ziweze kuelewa habari wanazopokea na kuwasiliana na shule. Ni lazima shule zihakikishe kwamba familia zote zinaelewa habari wanazoshiriki nazo. Ni lazima shule au wilaya lazima ziandae habari nyumbani katika lugha unayopendelea.

### Shule zinapaswa:

- Kuandaa ukalimani na utafsiri bila malipo katika matukio ya shule na mikutano.
- Kuuliza familia ni lugha gani wanayopendelea kutumia. Ni lazima shule iziombe familia zote zinazowaandikisha wanafunzi wapya kukamilisha Utafiti wa Matumizi ya Lugha.

Utafiti wa Matumizi ya Lugha ni fomu ambayo shule hutumia kujifunza kuhusu lugha ambazo familia huzungumza nyumbani. Huu unaweza kuzisaidia shule kuhakikisha kwamba zinashiriki habari katika lugha ambayo kila familia inataka. Hutumiwa pia kuwatambua wanafunzi ambao huenda wakahitaji utegemezo wa ziada wa lugha ya Kiingereza.

Ikiwa familia yako inazungumza lugha nyingine nyumbani, mtoto wako anaweza kuombwa kufanya jaribio ili kuona stadi zake za Kiingereza. Jifunze zaidi kwenye ukurasa wetu wa Utegemezo wa Lugha ya Kiingereza.

- Andaa fomu na habari katika lugha ambazo familia zinapendelea.

  **Muhimu:** Huenda familia isijihisi huru na mkalimani anayeandaliwa na shule. Wanaweza kuiomba shule iandae mkalimani tofauti. Shule haziwezi kumwomba mtoto au mshiriki wa familia yeyote akalimani kwa ajili ya shule. Ingawa familia zinaweza kuchagua kuwa na rafiki au mshiriki wa familia atumike kama mkalimani, ni muhimu kukumbuka kwamba mkalimani bila mafunzo huenda asijue maneno yote ya kielimu yanayotumiwa, na hilo linaweza kuongeza kutoelewana. Watoto ambao hukalimani kwa ajili ya wazazi au familia yao wanaweza pia kupata shinikizo na mkazo zaidi.

Jifunze zaidi kwenye ukurasa wetu wa kutumia wakalimani.

## Haki ya Kujifunza Kiingereza

Ni lazima shule ziandae utegemezo wa ziada kwa wanafunzi walio na shida kutumia Kiingereza shuleni. Shule zote zinapaswa kutumia mchakato uleule ili kujua ni wanafunzi gani wanaoweza kufaidika na msaada wa ziada wa lugha ya Kiingereza. Wanafunzi hawa huchukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu mchakato na jinsi shule hutoa msaada wa lugha ya Kiingereza kwa kutembelea ukurasa wetu wa Usaidizi wa Lugha ya Kiingereza.

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

### Kuna sheria kadhaa kuhusu jinsi shule zinavyowategemeza wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza:

- Ni lazima ziangalie stadi za lugha ya Kiingereza za wanafunzi wanaotumia lugha nyingine isipokuwa Kiingereza nyumbani. Hili huwasaidia kuamua ikiwa mwanafunzi atafaidika na kupokea msaada wa kuboresha ustadi wake wa Kiingereza.

  Ni lazima shule ziangalie stadi za Kiingereza za wanafunzi ndani ya siku 30 za kwanza baada ya mwanafunzi kuandikishwa shuleni. Zinafanya hivi kwa kuwafanya wanafunzi wakamilishe Kiwamba cha Ustadi wa Lugha ya Kiingereza cha Ohio. Ikiwa mwanafunzi atajiandikisha au kuhamia shule baada ya mwaka wa shule kuwa tayari umeanza, shule ina siku 45 za kuangalia stadi za Kiingereza za wanafunzi.
- Ni lazima shule zote katika Ohio zitumie jaribio lilelile ili kuona stadi za Kiingereza za wanafunzi Matokeo ya jaribio lazima yashirikiwe na familia.
- Ni lazima shule ijulishe familia ikiwa mwanafunzi wake ana alama chini ya Ustadi kwenye jaribio la Kiingereza linaloangalia stadi zake. (Mtihani wa Kiingereza utakuwa Kiwamba cha Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio au Tathmini ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya Ohio.)
- Familia huamua ikiwa inataka mtoto wao apokee utegemezo wa lugha ya Kiingereza au la.
- Utegemezo wa lugha ya Kiingereza unaweza kuwa tofauti, lakini lazima shule zihakikishe kwamba zinawasaidia wanafunzi kujifunza Kiingereza.
- Wanafunzi wanaofikiriwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza lazima wapokee utegemezo wanaohitaji ili kujifunza masomo mengine yote yanayofundishwa kwa Kiingereza shuleni.
- Wanafunzi hawapaswi kurudia darasa lilelile kwa sababu tu ni Mwanafunzi wa Kiingereza. Shule inapaswa kuzingatia maendeleo ya jumla ya kitaaluma ya mwanafunzi. Inapaswa pia kuzingatia maoni ya walimu na familia.

## Kujiandikisha katika Shule

Kuna haki fulani za kipekee wakati wa kuwaandikisha wanafunzi shuleni. Jifunze zaidi

kuhusu uandikishaji kwenye ukurasa wetu wa uandikishaji.

Wanafunzi wote wana haki ya kuhudhuria shule ya umma. Asili ya wanafunzi haibadilishi haki hii. Hii inatia ndani lugha ya nyumbani au stadi za Kiingereza.

### Shule zinapaswa:

- Kuandaa habari kuhusu uandikishaji kwa familia. Ni lazima iwe katika lugha ambayo familia huelewa vizuri kabisa. Hii ni pamoja na nyaraka zilizoandikwa.
- Kuandaa mkalimani ili kuzisaidia familia kuzungumza na shule.
- Kuandikisha wanafunzi wanaokabiliwa na ukosefu wa makazi mara moja. Hata kama familia haiwezi kuandaa ushahidi wa makazi.
- Shule haiwezi kuchelewesha uandikishaji kwa sababu ya hali ya utunzaji wa nyumbani au malezi.

  Tembelea ukurasa wa Utegemezo wa Wanafunzi kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) ili kujifunza zaidi.

### Familia zinapaswa kuandaa:

- Uthibitisho wa umri wa mtoto wao
- Nyaraka zinazoonyesha kwamba familia inaishi katika wilaya ya shule

  Familia zinapaswa kuandaa nyaraka zinazoonyesha mahali wanapoishi. Wanafunzi na familia zinazokabiliwa na ukosefu wa makazi zinaweza kuwa na machaguo mengine.
- Rekodi za chanjo

## Kulinda Faragha ya Familia Yako

Shule lazima zikusanye habari kuwahusu wanafunzi wote na familia zao. Hili huisaidia shule kuwa na rekodi sahihi. Shule hutumia habari hii kuandaa ripoti kwa serikali zinazozisaidia shule kuhudumia familia vizuri.

> **Muhimu:** Ni lazima shule zishiriki maelezo ya kibinafsi ya mwanafunzi zinapohitajika na sheria tu. Familia pia inaweza kupeana ruhusa kwa shule kushiriki habari. Shule

haziwezi kuziomba familia kuthibitisha hali yao ya uhamiaji. Familia hazihitaji kupeana kwa shule nyaraka za uhamiaji au nambari za usalama wa jamii.

### Maelezo ya kibinafsi ambayo lazima shule ilinde:

- Maelezo ya kibinafsi ambayo yanaweza kumweka mwanafunzi au familia katika hatari - Haya yanatia ndani kitambulisho cha mwanafunzi, nambari za usalama wa kijamii, picha, au habari nyingine.
- Hali ya uhamiaji ya mwanafunzi au washiriki wa familia - ikiwa familia itachagua kushiriki habari hii na shule
- Tarehe za kuzaliwa
- Mahali ambapo wanafunzi walizaliwa
- Anwani ya familia
- Maelezo ya mawasiliano ya familia wakati wa dharura
- Rekodi za kozi iliyokamilishwa na nakala za matokeo
- Barua rasmi kuhusu hali ya mwanafunzi shuleni
- Rekodi za nidhamu
- Rekodi za matibabu na afya kutoka shuleni
- Taarifa za mahudhurio
- Habari kuhusu shule alizoenda mwanafunzi huyo awali

## Kushiriki katika Programu na Shughuli Nyingine za Shule

**Shule haziwezi kuwatenga wanafunzi kwa kutegemea jinsi walivyo na ufasaha katika Kiingereza.** Ni lazima wanafunzi wote wawe na fursa sawa ya kujiunga na programu na shughuli. Hii ni pamoja na wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza.

Kwa mfano, ushauri wa shule, michezo, programu za sanaa, na shughuli nyingine zinazotolewa na shule nje ya wakati wa darasa huwasaidia wanafunzi kufanikiwa.

Ni lazima shule zihakikishe kwamba njia ambayo wanafunzi huchaguliwa kwa ajili ya programu na shughuli nyingine za shule ni ya usawa.

## Elimu ya Pekee

Wanafunzi fulani wanaweza kuhitaji huduma za pekee za elimu ikiwa watapata ugumu wa kujifunza.

Hii ni pamoja na wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza. Mtu yeyote anaweza kuiomba shule kumtathmini mwanafunzi kwa ajili ya elimu ya pekee. Hii ni pamoja na wazazi, walezi, washiriki wa familia, walimu, na wafanyakazi wengine wa shule. Wanafunzi wanaweza pia kujipendekeza.

## Shule zinapaswa:

- Kuamua ikiwa mtoto ana ulemavu. Hili hufanywa kwa tathmini. Familia au wafanyikazi wengine wa shule wanaweza kufikiri kwamba mwanafunzi ana matatizo ya kujifunza.
- Kamilisha tathmini katika maeneo yote ya uhitaji katika lugha ambayo mtoto anapendelea. Katika hali fulani, mkalimani anahitajika.
- Andaa habari kwa familia katika lugha wanayopendelea. Andaa ukalimani na utafsiri bila malipo inavyohitajika.
- Tengeneza mpango wa kutimiza mahitaji ya mwanafunzi. Mpango unapaswa kuzingatia mahitaji ya lugha ya mwanafunzi. Hili ni muhimu hasa kwa wanafunzi ambao ni Wanafunzi wa Kiingereza au wanaopokea msaada wa kuboresha ustadi wao wa Kiingereza.

Tembelea ukurasa wa Familia za Wanafunzi wenye Ulemavu kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) kwa habari zaidi kuhusu mchakato wa elimu ya pekee.

## Elimu ya Kuzawadiwa

Wanafunzi wa Kiingereza ambao hupata alama za viwango vya juu kuliko wanafunzi wenzao wanaweza kustahili huduma za elimu ya kuzawadiwa.

- Wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza wana haki ya kushiriki katika huduma za kuzawadiwa zinazoandaliwa na shule.
- Shule haziwezi kuwatenga wanafunzi kwa kutegemea tu jinsi walivyo na ufasaha katika

Kiingereza.

- Wanafunzi wote ambao wamerejelewa kwa utambulisho wa vipawa katika shule wanapaswa kujaribiwa. Jaribio linaonyesha kwamba wanaweza kupokea huduma za kuzawadiwa. Shule ina siku 90 za kumjaribu mwanafunzi.
- Mtu yeyote anaweza kuiomba shule kumjaribu mwanafunzi kwa elimu ya vipaji. Hii ni pamoja na wazazi, walezi, washiriki wa familia, walimu, na wafanyakazi wengine wa shule. Wanafunzi wanaweza pia kujipendekeza.

Tembelea ukurasa wa Uchunguzi wa Vipawa na Utambulisho wa Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) ili kujifunza zaidi.

### Masomo ya Mtandaoni

Haki za elimu kwa wanafunzi ni zilezile wanafunzi wanapojifunza mtandaoni. Ni lazima wanafunzi wanaofanya masomo ya mtandaoni wapate utegemezo uleule katika mafundisho ya lugha sawa na jinsi wangepokea ana kwa ana shuleni.

Jifunze zaidi kwenye ukurasa wetu wa masomo ya mtandaoni.

## Usalama katika Shule

Katika jimbo la Ohio, ni lazima shule ziwalinde wanafunzi wote dhidi ya unyanyasaji. Hii ni pamoja na kusumbuliwa na kutendewa vibaya shuleni. Hii inatumika kwa wanafunzi wanaochukuliwa kuwa Wanafunzi wa Kiingereza. Ni lazima shule zichukue hatua kuwalinda wanafunzi wanaonyanyaswa. Ni lazima wawazuie wanafunzi wasitende vibaya kuwaelekea wengine.

Unaweza pia kupiga simu kwa Nambari ya Kuripoti ya Shule ya Ohio iliyo Salama Zaidi (Safer Ohio School Tip Line) kwa 844-723-3764. Ni rasilimali ya usalama isiyo na malipo inayopatikana katika shule zote za Ohio. Nambari ya kuripoti ni mfumo wa kuripoti bila kutaja jina unaokubali maelezo kupitia simu, ujumbe, fomu ya wavuti, na programu ya rununu saa 24 kwa siku. Jifunze zaidi kwenye tovuti ya Kituo cha Usalama wa Shule cha Ohio.

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

## Vipi ikiwa shule haifuati masharti haya?

- Familia na shule zinaweza kutatua matatizo mengi pamoja. Ikiwa familia inafikiria kwamba shule haikidhi masharti au kuwatendea kwa usawa, wanapaswa kuzungumza na shule kwanza. Wanapaswa kujadili jinsi shule inavyoweza kumtegemeza mwanafunzi wao.
- Familia inaweza kuomba msaada kutoka kwa mfanyakazi wa shule, kama vile mwalimu wa Lugha ya Kiingereza.

  Mwalimu wa TESOL (Kufundisha Kiingereza kama Lugha Nyingine) au mwalimu wa ESL (Kiingereza kama Lugha ya Pili), uhusiano na familia au mshauri wa shule anaweza kusaidia.
- Ikiwa suala hilo litaendelea, familia inaweza kuwasiliana na mkuu wa shule.

  Wakuu wa shule husimamia shule na wafanyakazi wote katika jengo hilo.
- Ikiwa hakuna yeyote katika shule anayeweza kusaidia, familia inaweza kukutana na mkuu wa wilaya.

  Mkuu wa wilaya anasimamia huduma za Lugha ya Kiingereza katika shule zote za wilaya.
- Familia pia zinaweza kuwasiliana na Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) kwa msaada katika lau@education.ohio.gov.

Ikiwa familia haiwezi kurekebisha matatizo na shule moja kwa moja, wanaweza kuwasiliana na ofisi kutoka kwa serikali ya Marekani. Ofisi hizi zinaweza kuwasaidia wanafunzi ambao ni Wanafunzi wa Kiingereza na familia zao.

### Familia zinaweza kuwasiliana na:

- Ofisi ya Haki za Kiraia ya Idara ya Elimu ya Marekani (United States Department of Education's Office for Civil Rights (OCR)) kwa habari zaidi kuhusu kuwasilisha malalamishi.
- Kitengo cha Haki za Kiraia cha Idara ya Haki ya Marekani (The United States Department of Justice's Civil Rights Division) kwa habari zaidi kuhusu kuwasilisha malalamishi.

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University

Kwa masuala yanayohusiana na elimu ya pekee au elimu ya kuzawadiwa, familia zinaweza pia kuwasiliana na Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW). Familia zinaweza kuwasilisha malalamishi mtandaoni kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW).

## Maswali Unayoweza Kuuliza

- Je, tafadhali unaweza kueleza haki za elimu ni nini na kwa nini ni muhimu?
- Ikiwa nina mahangaiko au maswali kuhusu haki za elimu za mtoto wangu, ninapaswa kuwasiliana na nani na anaweza kunisaidiaje?
- Ninawezaje kuhakikisha kwamba haki za elimu za mtoto wangu zinaheshimiwa na kulindwa katika shule hii?
- Shule itahakikishaje kwamba mtoto wangu ana ufikiaji sawa wa fursa za elimu, bila kujali asili ya lugha yake?
- Je, kuna programu au huduma za kipekee zinazotolewa ili kusaidia wanafunzi wa lugha nyingi kufanikiwa kitaaluma?
- Walimu watatumia mikakati gani kutegemeza kujifunza na uelewaji wa mtoto wangu wa masomo wakati Kiingereza si lugha yake ya kwanza?
- Ninawezaje kuhusishwa kama mzazi katika kutegemeza na kutetea haki za elimu za mtoto wangu katika shule hii?

## Vifaa vya Ziada

### Haki za Familia

- Unaweza kujifunza zaidi kutoka kwa sehemu ya "Kuhudhuria Shule nchini Marekani" ya Vifaa vya Familia vya NCELA unapochagua Sura ya 2. Inapatikana katika lugha nne (Kiingereza, Kiarabu, Kichina, na Kihispania). https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit
- USA Hello huandaa habari zaidi kuhusu haki za familia na sheria nyingine za elimu. https://usahello.org/education/children/education-law-and-rights
- Ofisi ya Haki za Kiraia huandaa karatasi ya habari iliyo na maelezo kuhusu haki za familia

na Wanafunzi wa Kiingereza. https://www2.ed.gov/about/offices/list/ocr/docs/dcl-factsheet-el-students-201501.pdf

- USA Hello huandaa habari za jumla kuhusu haki za wahamiaji na wakimbizi. https://usahello.org/immigration/your-rights
- Karatasi ya habari ya Kituo cha Sheria ya Elimu huandaa muhtasari wa haki za Wanafunzi wa Kiingereza na familia za wanafunzi wenye ustadi mdogo wa Kiingereza. https://www.elc-pa.org/resource/rights-of-english-language-learners-families-with-limited-english-proficiency

### Mawasiliano Kati ya Familia na Shule

- Colorin Colorado huandaa viunganishi kwa karatasi ya habari kutoka kwa idara ya Elimu ya Marekani (US department of Education). Inajibu maswali ya kawaida kuhusu haki za familia ambazo hazizungumzi, kusikiliza, kusoma, au kuandika Kiingereza kwa ustadi kwa sababu si lugha yao ya kwanza. https://www.colorincolorado.org/guide/fact-sheet-information-limited-english-proficient-parents-and-schools-and-school-districts

### Usalama

- Unaweza pia kupiga simu kwa Nambari ya Kuripoti ya Shule ya Ohio iliyo Salama Zaidi (Safer Ohio School Tip Line) kwa 844-723-3764. Ni rasilimali ya usalama isiyo na malipo inayopatikana katika shule zote za Ohio. Nambari ya kuripoti ni mfumo wa kuripoti bila kutaja jina unaokubali maelezo kupitia simu, ujumbe, fomu ya wavuti, na programu ya rununu saa 24 kwa siku. Jifunze zaidi kwenye tovuti ya Ohio School Safety Center. https://ohioschoolsafetycenter.ohio.gov/pre-k-12-schools/safer-ohio-school-tip-line
- Unaweza kujifunza zaidi kutoka kwa sehemu ya "Afya na Usalama wa Mtoto Wako Shuleni" ya Vifaa vya Familia vya NCELA unapochagua Sura ya 5. Inapatikana katika lugha nne (Kiingereza, Kiarabu, Kichina, na Kihispania). https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit
- Jifunze zaidi kuhusu kuwalinda wanafunzi kutokana na unyanyasaji kwenye tovuti ya Colorin Colorado. https://www.colorincolorado.org/article/8-tips-protect-ells-bullying-

your-classroom-and-school

## Elimu ya Pekee

- Mwongozo wa Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) wa haki za wazazi huandaa habari zaidi kuhusu haki za familia katika elimu ya pekee. https://education.ohio.gov/Topics/Special-Education/A-Guide-to-Parent-Rights-in-Special-Education
- Tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) huandaa habari zaidi kwa familia kuhusu elimu ya pekee katika Ohio. https://education.ohio.gov/Topics/Special-Education/Families-of-Students-with-Disabilities

*Vifaa hivi vinalenga kuimarisha ustawi wa kitaaluma, wanafunzi na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa lugha nyingi wa Ohio. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi ya pamoja kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) na Kituo cha The Ohio State University cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE) pamoja na kikundi kilichojitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 